# Va, et toi, fais de même

Par James E. Evanson
*des soixante-dix*

# Nenda na Ukatende Vivyo Hivyo

Na Mzee James E. Evanson
*Wa Sabini*

Conférence générale d’octobre 2025

*J’aimerais mettre en lumière le rôle des missionnaires appelés à faire une mission dédiée au service. Ils sont des exemples pour nous.*

*Ningependa kuangazia wale wamisionari waliopangiwa kazi ya kutoa huduma. Wao ni mifano kwetu.*

Tandis que le Sauveur parcourait la région de Bethsaïda, quelques personnes lui ont amené un aveugle. Celles-ci espéraient peut-être être les témoins directs d’un miracle. Le Sauveur « prit l’aveugle par la main et le conduisit hors du village » afin de le guérir en privé. Cette guérison n’a d’abord pas semblé efficace. L’homme regarda et dit : « J’aperçois les hommes, mais je les vois comme des arbres qui marchent. » Avec compassion, Jésus « lui mit de nouveau les mains sur les yeux ; et, quand l’aveugle regarda fixement », grâce à ce geste supplémentaire du Sauveur, « il […] vit tout distinctement».

Cela n’est qu’un exemple parmi d’autres de la façon dont la vie du Sauveur se caractérise par d’humbles actes de service. Il nous rappelle qu’il « est venu, non pour être servi, mais pour servir», et il nous invite ensuite à suivre son exemple en faisant le deuxième mille, donnant à celui qui nous demandeet aimant notre prochain. Lorsqu’on lui a demandé : « Qui est mon prochain ? » Le Christ a raconté la parabole du bon Samaritain, avec le commandement suivant : « Va, et toi, fais de même. »

Les missionnaires de l’Église de Jésus-Christ des Saints des Derniers Jours sont des exemples modernes du bon Samaritain que le Christ nous invite à devenir. J’aimerais mettre en lumière le rôle des missionnaires appelés à des missions dédiées au service. Ils sont pour nous des exemples de la manière dont le service (1) ouvre les cœurs à l’Évangile de Jésus-Christ, (2) nous permet à tous de servir quelle que soit notre

Wakati Mwokozi alipokuwa akisafiri kupitia Bethsaida, baadhi ya watu walimleta mtu asiyeona Kwake. Pengine walikuwa wakitarajia kuona muujiza papo hapo. Mwokozi “alimchukua yule mtu asiyeona kwa kumshika mkono, na kumwongoza nje ya mji” ili kumponya kwa faragha. Mwanzoni, uponyaji ulionekana kuwa usio wa ufanisi sana. Yule mtu “akatazama juu, na akasema, ninaona watu kama miti ikitembea.” Yesu, kwa huruma, “aliweka mikono yake tena juu ya macho yake, na kumfanya aangalie juu.” Na kwa ule mguso wa ziada wa mikono ya Mwokozi, mtu yule asiyeona sasa “aliona … wazi kabisa.”

Huu ni mfano mmoja tu wa jinsi maisha ya Mwokozi yanavyofahamika kwa vitendo vya unyenyekevu vya huduma. Anatukumbusha kwamba Yeye “hakuja kutumikiwa, bali kutumikia”na kisha anatualika kufuata mfano Wake kwa kwenda maili ya ziada,tukitoa kwa wale wanaotuomba,na kuwapenda jirani zetu.Yeye alipoulizwa, “Na jirani yangu ni nani?” Kristo alishiriki mfano wa Msamaria mwema kwa wito wa “nenda, na ukatende vivyo hivyo.”

Wamisionari wa Kanisa la Yesu Kristo la Watakatifu wa Siku za Mwisho ni mfano wa siku za sasa wa Msamaria mwema ambao Kristo anatualika sisi tuwe. Ningependa kuangazia wale wamisionari walio pangiwa kazi ya kutoa huduma.Wao ni mifano kwetu sisi wa jinsi huduma (1) inavyofungua mioyo kwa injili ya Yesu Kristo, (2) inavyoruhusu sisi sote kutumikia bila kujali hali zetu, na (3) inavyoleta nguvu ya Kristo ndani

situation et (3) attire le pouvoir du Christ dans notre vie.

## Premièrement, le service ouvre les cœurs à l'Évangile de Jésus-Christ

Vers 91 av. J.-C., Ammon, un missionnaire du Livre de Mormon, s'est présenté au roi Lamoni en disant : « Je désire demeurer un certain temps parmi ce peuple ; [et] je serai ton serviteur. » Grâce à la façon dont il a servi le roi, Ammon a eu l'occasion de « parler hardiment, et [de dire au roi Lamoni] par quel pouvoir » il a accompli ces choses. En contrepartie, le roi a promis à Ammon : « Tout ce que tu désires, je te le donnerai. » La seule requête d'Ammon a été que le roi écoute le message de l'Évangile de Jésus-Christ. Le service d'Ammon a eu pour résultat « d'amener des milliers d'âmes au repentir».

De nos jours, le service continue de conduire les gens à l'Évangile. Sœur Bevan faisait une mission dédiée à l'enseignement lorsqu'elle a commencé à rencontrer des problèmes de santé nécessitant son retour chez elle pour suivre un traitement. Au lieu d'être relevée, elle a pu continuer de servir dans le cadre d'une mission dédiée au service depuis chez elle.

Alors qu'elles traversaient un parc, sœur Bevan et une amie se sont senties poussées à parler à une mère accompagnée de ses quatre jeunes enfants, mais elles ont hésité et la famille s'en est allée. Le lendemain, elles sont retournées dans ce parc, priant pour que la famille s'y trouve aussi. Miraculeusement, la mère était assise exactement au même endroit que la veille. Cette fois, sœur Bevan et son amie sont allées lui parler et, tout en faisant connaissance avec elle, ont découvert qu'elle avait désespérément besoin d'une aide temporelle. Elles lui ont apporté leur soutien et l'ont ensuite invitée à découvrir l'Évangile.

Grâce à ce service et à cette invitation, la mère et l'aîné des enfants se sont fait baptiser, suivi du cadet un an plus tard. Ils sont toujours pratiquants aujourd'hui. Sœur Bevan savait que cette expérience était divinement inspirée et cela lui a prouvé qu'elle se trouvait exactement à l'endroit où Dieu avait besoin qu'elle soit.

Comme Ammon et sœur Bevan, lorsque nous servons autrui, nous « [lui donnons] le bon

ya maisha yetu.

## Kwanza, Huduma Inafungua Mioyo kwa Injili ya Yesu Kristo

Karibia mwaka wa 91 K.K, Amoni, Mmisionari wa Kitabu cha Mormoni, alijitambulisha mwenyewe kwa Mfalme Lamoni kwa kusema, “Ninatamani kuishi miongoni mwa watu hawa kwa muda; … [nami] nitakuwa mtumishi wako.”Kwa sababu ya huduma yake kwa mfalme, Amoni alipewa fursa ya “kuzungumza kwa ujasiri, …na kumwambia [Mfalme Lamoni] … kwa uwezo gani” yeye alitenda huduma yake.Katika majibu, mfalme aliahidi kwamba “lo lote [Amoni] atakalotaka … [mfalme ange]mpatia.”Ombi pekee la Amoni lilikuwa kwamba mfalme asikilize ujumbe wa injili ya Yesu Kristo.Matokeo ya huduma ya Amoni ilikuwa “maelfu ya roho [zililetwa] kwenye toba.”

Katika siku yetu, huduma inaendelea kuwaongoza wengine kwenye injili. Dada Bevan alikuwa anahudumu kama mmisionari wa kufundisha wakati alipoanza kupitia matatizo ya kiafya yaliyomhitaji yeye kurudi nyumbani kwa ajili ya matibabu. Badala ya kupumzishwa, yeye aliweza kuendelea kuhudumu kama mmisionari wa kutoa huduma akitokea nyumbani.

Wakati wakitembelea bustani, Dada Bevan pamoja na rafiki yake walishawishiwa kuzungumza na mama akiwa na watoto wadogo wanne, lakini walisita mpaka ile familia ikaondoka. Siku iliyofuata, walirudi kwenye ile bustani, wakisali kwamba familia hii ingekuwa pale. Kwa muujiza, mama yule alikuwa amekaa mahali pale pale kama siku ya jana. Wakati huu Dada Bevan na rafiki yake walimwendea yule mama, wakapata kumjua, na wakagundua kwamba alikuwa na haja ya msaada wa kimwili. Walitoa ule msaada na kisha wakamwalika kujifunza kuhusu injili.

Kwa sababu ya huduma hiyo na mwaliko, mama huyu na mtoto wake mkubwa walibatizwa, wakifuatiwa na mtoto aliyefuatia kwa ukubwa mwaka mmoja baadaye. Bado waumini hai hadi leo hii. Dada Bevan alijua uzoefu wake ulishawishiwa kiungu, na “ilithibitika [kwake] kwamba [yeye] alikuwa mahali pale pale Mungu alipohitaji [yeye] awepo.”

Kama Amoni na Dada Bevan, tunapo wahudumia wengine, sisi “tunaonyesha mfano

exemple» et il désire connaître la « raison de l'espérance qui est en [nous]».

Jésus nous lance cette invitation : « Va, et toi, fais de même. »

## Deuxièmement, le service nous permet à tous de servir quelle que soit notre situation

Le président Nelson a demandé à «chaque-jeune homme digne et apte de se préparer pour une mission, et d'en faire une », et à chaque sœur jeune et capable de « [prier] pour savoir si le Seigneur désire [qu'elle fasse] une mission ». Il a promis : « Votre décision de faire une mission, qu'elle soit de prosélytisme ou [dédiée au] service, sera une bénédiction pour vous et pour beaucoup d'autres. » Les missions dédiées au service ont transformé la définition du motcapable. À présent, chaque jeune homme et chaque jeune femme qui désirent faire une mission à plein temps pour le Seigneur le peuvent, à de très rares exceptions.

Quand il s'agit de servir indépendamment de notre situation personnelle, elder Holgado est un exemple. Il est né avec une maladie génétique rarequi l'empêchait de faire une mission dédiée à l'enseignement. Elder Holgado a été appelé en tant que missionnaire dédié au service et a effectué du bénévolat au sein du magasin de l'évêque, permettant à des centaines de personnes de recevoir le soutien dont elles avaient besoin. Il garnissait les étagères, emballait les légumes et compactait les cartons.

Prenant la parole à la réunion de Sainte-Cène après sa mission, elder Holgado a déclaré : « Dieu a besoin de missionnaires dédiés au service. Il a besoin de gens qui aiment et servent autrui. Ces personnes entreposent du papier hygiénique, emballent des brocolis, montent des meubles et font du bien aux gens. »

Vous n'avez pas besoin de recevoir une tâche de service ou de porter un badge missionnaire pour faire du bien. Le Sauveur reconnaît chaque acte de service. Nous sommes tous capables d'aider les gens à venir au Christ en les servant avec amour et gentillesse. Nous pouvons tous servir chaque personne individuellement au nom du Christ, par le pouvoir du Saint-Esprit, et mener une vie exemplifiant la foi en Jésus-Christ. Le service nous permet de nous présenter comme

mwema kwao"na wanatamani kujua "sababu ya tumaini lililoko ndani yetu [sisi]."

Yesu anatualika "nendeni, nanyi mkatende vivyo hivyo."

## Pili, Huduma Inaturuhu Kutumikia Bila Kujali Hali Zetu

Rais Russell M. Nelson alitoa wito juu ya "kila mvulanamwenye kustahili, anayeweza ili kujiandaa kwa ajili ya na kuhudumu misheni" na kwa kila msichana anayeweza "kusali ili kujua kama Bwana angependa [yeye] ahudumu misheni." Aliahidi kwamba "uamuzi wako wa kuhudumu misheni, iwe ya kufundisha au misioni ya kutoa huduma, utakubariki wewe na wengine wengi."Misheni za kutoa huduma zimebadilisha maana ya nenoweza.Sasa kila mvulana mwenye kustahili na msichana anayetamani kuhudumu kama mmisionari kwa ajili ya Bwana anaweza kufanya hivyo, isipokuwa wachache sana.

Mze Holgado ni mfano wa kuwa na uwezo wa kuhudumu bila ya kujali hali binafsi. Yeye alizaliwa na maradhi ya kurithi yasiyo ya kawaida,ambayo yalimtenga na kuhudumu kama mmisionari wa kufundisha. Mzee Holgado aliitwa kama mmisionari wa kutoa huduma na alijitolea kufanya kazi katika ghala ya askofu, mahali ambapo aliwasaidia wengine kupata msaada walio hitaji. Yeye alipanga safu, aliweka mboga katika maboksi, na kuvunja maboksi ya kadibodi.

Mzee Holgado alipokuwa akizungumza katika mkutano wa sakramenti baada ya misheni yake, alishiriki kwamba "Mungu anahitaji wamisionari wa kutoa huduma. Anahitaji watu wa kuwapenda na kuwahudumia wengine. Watu hawa hupanga karatasi za maliwato, kupakia brokoli kwenye mifuko, kujenga samani, na ni watu walio wema kwa watu."

Huhitaji kupangiwa kazi ya kuhudumu au kuvaa tagi ya jina ili kufanya yaliyo mema. Kila tendo la huduma hutambuliwa na Mwokozi. Sisi sote tunaweza kuwasaidia wengine kuja kwa Kristo kwa kuhudumu kwa upendo wa ukarimu. Sisi sote tunaweza kutumikia katika jina la Kristo kwa yule mmoja kupitia uweza wa Roho Mtakatifu na kuishi kama mifano ya imani katika Yesu Kristo.Huduma inaturuhusu sisi kujiwasilisha wenyewe kama dhabihu inayo ishi ambayo in-

des sacrifices vivants, agréables à Dieu.

Jésus nous lance cette invitation : « Va, et toi, fais de même. »

## Troisièmement, le service attire le pouvoir du Christ dans notre vie

Un jeune missionnaire, qui avait été transféré d'une mission dédiée à l'enseignement à une mission dédiée au service, a rencontré certaines difficultés personnelles suscitant chez lui le besoin du pouvoir guérisseur du Christ. Le service consacré a apporté ce pouvoir dans sa vie. Il a dit : « J'ai ressenti, pendant que je traversais ces difficultés, que le Christ me soutenait. Il y a vraiment quelque chose de spécial à le voir bénir les gens dans une banque alimentaire, dans le temple ou encore grâce à son Évangile. »

Ce frère a commencé à éprouver une joie plus profonde, et son enthousiasme renouvelé s'est avéré une bénédiction pour lui et toute sa famille. L'Esprit a pénétré plus abondamment leur foyer, ils sont allés au temple ensemble plus régulièrement et le Christ a occupé une place plus importante au sein de leur famille. Ce missionnaire croit que le Christ a sauvé sa vie et béni sa famille grâce au service.

Le président Nelson a enseigné : « Le désir de servir et d'affermir autrui est un symbole de notre empressement à être guéris » par le pouvoir rédempteur du Sauveur.

Jésus nous lance cette invitation : « Va, et toi, fais de même. »

## Les missionnaires dédiés au service sont des exemples de disciples consacrés de Jésus-Christ

Quand vous, ou un membre de votre famille, êtes appelés comme missionnaire dédié au service, c'est un moment à célébrer. Dès lors, votre famille comptera un représentant du Seigneur Jésus-Christ qui a été mis à part et qui demeure au sein du foyer. Cela vous transformera tous pour le bien. Un appel à servir ne devrait jamais susciter de déception. Nous chantons ces paroles : « J'irai où tu veux que je sois, ce que tu voudras je serai. » Voici une occasion de montrer que nous croyons vraiment ce que nous disons !

Vous tous qui servez, et plus spécialement les quatre mille jeunes missionnaires dédiés au service, nous vous aimons ! Si les missionnaires dédiés à l'enseignement sont la bouche du Sei-

akubalika kwa Mungu.

Yesu anatualika "nendeni, nanyi mkatende vivyo hivyo."

## Tatu, Huduma Huleta Nguvu za Kristo Ndani ya Maisha Yetu

Mmisionari kijana aliyepewa uhamisho kutoka jukumu la kufundisha kuwa jukumu la kutoa huduma alipambana na baadhi ya changamoto binafsi ambazo zilimwacha akihitaji nguvu ya Kristo ya uponyaji. Huduma iliyowekwa wakfu ilileta nguvu hiyo ndani ya maisha yake. Yeye alisema, "Nilihisi kwamba wakati nilipokuwa nikipambana, niliweza kumhisi Kristo akininyanyua juu. Kuna kitu fulani maalumu kuhusu kumwona Yeye akiwabariki watu kupitia stoo ya chakula, ndani ya hekalu, na kupitia injili Yake."

Mzee huyu alianza kuhisi shangwe ya kina, na hamasa mpya aliyoigundua ilimbariki yeye na familia yake yote. Roho aliingia ndani ya nyumba yao kwa wingi sana, walihudhuria hekaluni pamoja zaidi mara kwa mara, na Kristo akawa fokasi kuu katika familia yao. Mmisionari huyu anaamini kwamba Kristo aliokoa maisha yake na aliibariki familia yake kupitia huduma.

Rais Nelson alifundisha, "Utayari wa kuhudumu na kuwaimarisha wengine vinasimama kama ishara ya utayari wa mtu kuponywa" kwa nguvu za Mwokozi zenye kukomboa.

Yesu anatualika sisi "nendeni, nanyi mkatende vivyo hivyo."

## Wamisionari wa Kutoa Huduma ni Mifano ya Wanafaunzi wa Yesu Kristo Walio Wekwa Wakfu.

Wakati wewe au mshiriki wa familia anapobarikiwa kupata wito kama mmisionari wa kutoa huduma, huo ni wakati wa kushangilia.Familia yako sasa itakuwa na mwakilishi wa Bwana Yesu Kristo aliyesimikwa akiishi ndani ya nyumba Yenu. Hiyo itawabadilisha ninyi nyote kuwa wema. Hakupaswi kuwa na kubeza katika wito wo wote wa kuhudumu. Tunaimba, "Nitakwenda utakako" na "Nitakuwa utakacho."Hii ni fursa ya kuonyesha kwa hakika tunamaanisha kile tunachosema!

Kwenu ninyi nyote mnaohudumu, na mahususi kwa wamisionari vijana 4,000 mnaotoa huduma, sisi tunawapenda! Kama wamisionari wa kufundisha ni vinywa vya Bwana, basi ninyi

gneur, alors les missionnaires dédiés au service sont ses mains, et vous n'êtes pas des missionnaires de seconde classe. Chacun de vous joue un rôle vital dans le rassemblement d'Israël. Le président Nelson a enseigné : « Chaque fois que nous faisons quoi que ce soit qui aide qui que ce soit […] à contracter et à respecter ses alliances avec Dieu, nous aidons à rassembler Israël. »

Vous, missionnaires dédiés au service, rassemblez Israël chaque jour de nombreuses manières différentes et votre service transforme des vies. Il arrive souvent que vous ne sachiez pas à qui profitent vos actes de service, mais Dieu le sait. Souvenez-vous toujours que « toutes les fois que vous [servez] l'un de ces plus petits, [c'est lui que] vous [servez]». Nous entendons vos voix lorsque vous êtes bénévoles dans les centres d'appel de l'Église, nous voyons vos sourires lorsque vous aidez au sein d'organisations de la collectivité et nous percevons votre lumière lorsque vous servez dans les temples. Vous donnez à manger à ceux qui ont faim, des vêtements à ceux qui sont nus et à boire à ceux qui ont soif.

Nous devons tous aller et faire de même.

## Le service est la force vive des disciples du Christ

Le service a le pouvoir d'ouvrir les cœurs à l'Évangile et nous permet à tous d'offrir notre âme tout entière au Christ. Il change notre cœur afin que nous devenions plus semblables à lui et, ce faisant, nous édifions autrui. Le président Nelson a un jour demandé : « Dans ce monde frappé de dépérissement spirituel, les personnes […] peuvent-elles faire changer les choses ? » Sa réponse est : « Oui ! […] 'Le peuple de l'alliance du Seigneur, armé de justice et du pouvoir de Dieu dans une grande gloire' […] peut améliorer la vie de tous les humains. » Par le service, nous changeons les cœurs et le monde.

Le Christ « allait de lieu en lieu faisant du bien». Il a guéri les malades, rendu la vue aux aveugleset ressuscité les morts. Il a préparé des repas, apporté son aide lors de noces de mariageet nourri des milliers de gens qui avaient faim. En rendant service à chacun au nom du Christ, nous devenons de plus en plus saints et dignes du don de la vie éternelle. Jésus-Christ vit. Il est mon Sauveur et le vôtre. Il est notre Rédempteur. Il est notre grand exemple de service. Je nous invite tous à aller et à faire de même.

wamisionari wa kutoa huduma ni mikono ya Bwana, na siyo wamisionari wa daraja la pili.Kila mmoja wenu ni muhimu sana katika kukusanya Israeli. Rais Nelson alifundisha kwamba "wakati wo wote tunapofanya kitu cho chote ambacho kinamsaidia mtu yeyote … kufanya na kushika maagano yao na Mungu, tunasaidia kukusanya Israeli."

Ninyi wamisionari wa kutoa huduma mnakusanya Israeli katika njia nyingi, na huduma yenu inabadilisha maisha. Mara nyingi wewe hujui mnufaika wa huduma yako ni nani, lakini Mungu anajua. Daima kumbuka kwamba "kadiri [umhudumiavyo] mmoja wa wadogo hawa, … [umemhudumuia Yeye]."Tunasikia sauti zenu mnapojitolea kwenye vituo vya huduma vya Kanisa; tunaona tabasamu zenu mnaposaidia katika vikundi vya jumuiya na tunahisi nuru yenu mnapohudumu katika mahekalu. Mnawalisha wenye njaa, mnawavisha walio uchi, na mnawapa kinywaji wenye kiu.

Sisi sote tunahitaji kwenda, na kutenda vivyo hivyo.

## Huduma ni Damu ya Uhai wa Wanafunzi wa Kristo.

Huduma inayo nguvu ya kufungua mioyo kwa ajili ya injili na inaturuhusu sisi sote kutoa nafsi yetu yote kwa Kristo.Huibadilisha mioyo yetu ili iwe kama Yeye, na katika mchakato, tunawainua wengine. Rais Nelson wakati mmoja alisema, "Katika ulimwengu huu uliopigwa kwa uozo wa kiroho, je, inawezekana watu … wakafanya tofauti?" Jibu lake: "Ndiyo! … 'Watu wa agano wa Mungu, … waliovikwa silaha … na nguvu za Mungu katika utukufu mkuu' … wanaweza kuinua maisha ya wanadamu wote."Kupitia huduma tunabadilisha mioyo—na huu ulimwengu.

Kristo "alizunguka huko na huko akitenda wema."Aliwatumikia wagonjwa,alirejesha uoni kwa vipofu,na kuwatembelea walio kataliwa.Alipika vyakula,alisaidia katika sherehe za harusi,na akawalisha maelfu wenye njaa.Tunapohudumu katika jina la Kristo kwa yule mmoja, tunazidi kuwa watakatifu na wenye kustahili zawadi ya uzima wa milele.Yesu Kristo yu hai. Yeye ni Mwokozi wangu na wako. Yeye ni Mkombozi wetu. Yeye ni mfano wetu mkuu wa utumishi. Ninakualikeni kila mmoja wetu twende, na

Au nom de Jésus-Christ. Amen.

tutende vivyo hivyo. Katika jina la Yesu Kristo, amina.